



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE

Kumb.Na.CA/92/112/149/01/0011'

Tarehe: 03.01.2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA WA MIEZI 12

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale anakaribisha maombi ya kazi ya Ajira ya Mkataba wa muda wa miezi 12 kwa kada ya Tabibu Msaidizi, Muuguzi II na Katibu Mhsusi III, hii ni kutokana na programu ya COMMUNITY, SOCIAL RESPONSIBILITY (CSR) inayotolewa na Mgodu wa Uchimbaji Zahabu wa Bulyanhulu kama ifuatavyo;

1. TABIBU MSAIDIZI (NAFASI 05) - Ngazi ya Mshahara TGHS A

(a) SIFA ZA MWOMBAJI:

Kuajiriwa wenye Cheti cha Mthani wa Taifa wa Kidato cha IV ambao wamehitimu Mafunzo ya Miaka Miwili ya Tabibu Wasaidizi (Clinical Assistants Certificate).

(b) KAZI NA MAJUKUMU:

- Kutoa huduma za Kinga na Tiba
- Kutambua na kutibu magonjwa
- Kutoa huduma ya Afya ya msingi (Primary Health Care)
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

2. MUUGUZI II (NAFASI 05) - Ngazi ya Mshahara TGHS A

(a) SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

(b) KAZI NA MAJUKUMU

- (i) Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya.
- (ii) Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi
- (iii) Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi
- (iv) Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani.

- (v) Kutoa ushauri nasaha
- (vi) Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango
- (vii) Kutoa huduma za uzazi na afya ya mtoto
- (viii) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
- (ix) Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
- (x) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

3. KATIBU MAHSUSI (NAFASI 01) - Ngazi ya Mshahara TGS B

SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha IV waliohudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu. Wawe wamefaulu somo la Hati mkato ya kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya Komputa kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali na kupata cheti katika program za WINDOWS, MICROSOFT OFFICE, INTERNET, EMAIL NA PUBLISHER.

KAZI NA MAJUKUMU

- a. Kuchapa barua, tarifa na Nyaraka za kawaida
- b. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- c. Kusaidia kutunza tarifa, kumbukumbu za matukio, miradi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi nyingine.
- d. Kusaidia kutafuta na kumtia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo Ofisini.
- e. Kutekeleza kazi zozote atakazo kuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.

MASHARITI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

- A. Waombaji wote wawe na Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
- B. Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI
- C. Waombaji waambatanishe Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni aidha Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- D. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.
- E. Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) HAVITAKUBALIWA.
- F. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).

G. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria

H. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 12 Januari, 2022


I. Maombi yawasilishwe kwa njia ya barua kwa:

Mkurugenzi Mtendaji

Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale

S.L.P 352

NYANG'HWALE.



David Rwazo

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)

NYANG'HWALE

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Nyang'hwale, S. L. P. 352, Mkoa wa Geita, Barua

pepe:ded@nyanghwaledc.go.tz Tovuti: www.nyanghwaledc.go.tz